


# HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W))

MKOA WA RUVUMA

Anwani ya Simu: "NYASA  
COUNCIL"  
Ofisini Simu Na: 025 -2952003  
Fax Na: 025 -2952005  
Nyumbani: 025 -  
Barupepe:- ps.ded@nyasad.go.tz



OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W),  
S. L. P. 90,  
**MBAMBA-BAY,  
RUVUMA.**

**25/06/2019.**

## TANGAZO

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA ANAWATANGAZIA WAFANYABIASHARA WOTE AMBAO LESENI ZAO ZA BIASHARA ZITAISHA MUDA WAKE TAREHE 30/06/2019, KUWA MSIMU MPYA WA KUHUIISHA LESENI ZA BIASHARA UTAANZA TAREHE 01/07/2019.

MUDA WA KULIPA KWA HIYARI NI KUENZIA TAREHE 01/07/2019 HADI TAREHE 21/07/2019. HIVYO MTATAKIWA KUFIKA KATIKA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI(W) MKIWA NA NYARAKA ZIFUATAZO ILI MUWEZE KUPATA LESENI KWA WAKATI:-

1. **CHETI CHA MLIPA KODI** (TAX CLEARANCE CERTIFICATE) KUTOKA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA).
2. NAKALA YA LESENI YA KIPINDI KILICHOPITA.

AIDHA KWA WAOMBAJI WAPYA WATAKIWA KUWA NA;

1. **HATI YA UTHIBITISHO WA URAIA** KAMA VILE (CHETI CHA KUZALIWA, KITAMBULISHO CHA UTAIFA, KADI YA MPIGA KURA AU HATI YA KIAPO KUTOKA MAHAKAMANI).
2. **HATI YA KUJIANDIKISHA KAMA MLIPA KODI (TIN)** KUTOKA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA) - MBINGA.
3. **CHETI CHA MLIPA KODI** (TAX CLEARANCE CERTIFICATE) KUTOKA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA) – MBINGA.

WAOMBAJI WOTE MTATAKIWA KUJAZA FOMU YA MAOMBI YA LESENI YA BIASHARA INAYOTOLEWA KATIKA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI(W).

Jimson P. Mhagama

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

